
# SADAKA YA UKARIMU

MARTIN MUTUA MUNYWOKI
*Kakumuti Kitui*
*25th Dec 2014*
*edited 2019*


♩ = 81






## MASHAIRI




***Jiandae wiki nzima weka tayari sadaka yako mkristu (jiulize)***
***Umepata nini, umebeba nini, utatoa nini***
***{Umtolee Mungu alicho kupa hahitaji zaidi (tazama)***
***Vitu vyote mali yake toa kwa ukarimu } *2***

1. Ninaona hasara kutoa (nanung'unika) Bwana ona, mimi nilivyopungukiwa,
Mara nyingi naomba jirani (hapa kitini) siyo yangu, ni sadaka ya kuazima

2. Ninaona ugumu kutoa (sadaka yangu) ninaleta, kidogo tena  kwa uchungu
Mara nyingine sitoi kitu (nilicho nacho) nahifadhi, kwa mahitaji yangu mengi

3. Ninaona aibu kubaki (ni wasiwasi) nimeketi, nao wengine wanatoa
Mara nyingine hata siendi (nimekimbia) kanisani,  ninahepa michango mingi

4. Wana heri wale watoao (kwa moyo ule) wa Abeli, wa Ibrahimu na Isaka
Bwana Mungu hapendi sadaka (yake Kaini) wala ile, ya Anania na Safira